Chama cha siasa ni lazima uanachama wa wanachama wake uwe ni wa hiari na uwe ni kwa raia wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.Chaa cha siasa kinatakiwa kujiepusha na ;-

i. Ubaguzi wa jinsi;
ii. Imani ya dini;
iii. Rangi;
iv. Asili;
v. Kabila;
vi. Taaluma au kazi;na
vii. Uchaguzi wa viongozi wake katika chaguzi zote uruhusu jinsi zote.

Chama cha siasa hakitasajiliwa ikiwa Katiba, kanuni, sera au shughuli za chama hicho zitakuwa zinajielekeza katika;

i. Kuvunja Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
ii. Matumizi ya nguvu au vurugu kama njia yake ya kufikia malengo yake ya kisiasa
iii. Kutekeleza malengo yake ya kisiasa katika upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
iv. Hauruhusu chaguzi za vipindi au demokrasia ya kuchagua viongozi wake;
v. Kuruhusu viongozi au wanachama wake kutumia lugha za matusi, dhihaka au kejeli ambazo zinaweza kusababisha uvunjifu wa amani.

## 7.0 Wajibu Wa Vyama Vya Siasa

Kila chama cha Siasa kinatakiwa kuwa na rejista ya wanachama wake; viongozi wa chama katika ngazi zote za uongozi;na wanachama katika vyombo vya chama katika kila ngazi ya uongozi.
Msajili wa vyama vya siasa ameruhusiwa na Sheria hii kuomba kwa maandishi Rejista tajwa. Chama kitakachoshindwa kupeleka rejesta hiyo pale itakapoombwa na Msajili kinaweza kusimamishwa na kiongozi wake atakuwa ametenda kosa na adhabu yake ni faini isiyopungua shillingi 1,000,000/= na isiyozidi shillingi 3,000,000/= au kifungo cha muda usiyopungua miezi mitatu au kisichozidi miezi sita au adhabu zote kwa pamoja.

- **Chama kilicho na usajili wa kudumu kinatakiwa kuwa na nyaraka zifuatazo-**

i. Sera ya jumla ya chama inayoelezea falsafa ya chama;
ii. Sera jumuishi ya chama kuhusu jinsi na ushirikishwaji wa jamii;
iii. Kanuni za chama kuhusu usimamizi ambazo zitaweza kusomwa na watu wenye mahitaji maalum;
iv. Kanuni za usimamizi wa fedha na mali za chama;
v. Kanuni za maadili za chama;
vi. Kanuni za uchaguzi wa ndani kuhusu uteuliwaji na uchaguzi wa viongozi wa chama;
vii. Kanuni za manunuzi za vyama vya siasa; na
viii. Kanuni za kuajiri za chama.

- **Chama cha siasa, kiongozi au mwanachama hatakiwi kusajili au kuunda kikundi cha ulinzi cha aina yoyote au kuwa na kikundi chenye lengo la kutekeleza kazi za Jeshi la Polisi au chombo chochote cha usalama cha Serikali.**

- **Chama cha siasa hakitakiwi kufanya, kufadhili, kuratibu au kutoa amri ya kuratibu mafunzo ya kijeshi au mafunzo yoyote ya namna ya kutumia nguvu au silaha kwa wanachama wake au mtu mwingine yeyote. Chama cha Siasa kitakachofanya hivyo kitakuwa kimetenda kosa na adhabu yake ni kufutwa na kila kiongozi, mwanachama wa chama husika atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka miaka ishirini.**

- **Chama kilichopata usajili wa kudumu kinatakiwa kuwa na bodi ya wadhamini**

## HITIMISHO

Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 imetoa masharti mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha demokrasia inakuzwa nchini. Vilevile Sheria hii imetoa wajibu kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, vyama vya siasa, viongozi na wanachama ili kuhakikisha demokrasia inakua bila kuathiri amani na utulivu wa nchi.

---

**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



# SHERIA YA VYAMA VYA SIASA SURA YA 258

## SHERIA YA VYAMA VYA SIASA SURA YA 258

### 1. 0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980, kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kuanzishwa kwa sheria hizo yanafikiwa. Aidha Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki katika maboresho ya sheria.

Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 inaanzisha Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa. Ofisi hii inasimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye anateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi hii pia ina manaibu wasajili.

### 2.0 Majukumu ya Msajili wa Vyama vya Siasa

Majukumu ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni pamoja na;-

i. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258;
ii. Kusimamia chaguzi na teuzi za ndani za vyama vya siasa;
iii. Kutoa miongozo na kusimamia mapato na matumizi ya vyama vya siasa na uwajibikaji kuhusu rasilimali za vyama vya siasa;
iv. Kutoa elimu ya uraia kuhusu demokrasia ya vyama vingi, sheria zinazosimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa;
v. Kusimamia elimu ya uraia inayotolewa kwa vyama vya siasa;
vi. Kuishauri Serikali kuhusu masuala ya vyama vya siasa;
vii. Kuwezesha mawasiliano baina ya vyama vya siasa na Serikali; na
viii. Kufanya tafiti kuhusu vyama vya siasa, demokrasia ya vyama vingi na ufadhili wa vyama vya siasa.

#### • Usimamizi wa Elimu ya Uraia

Sheria inainisha kuwa taasisi au mtu yeyote ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa anataka kutoa elimu ya uraia au mafunzo yoyote kwa chama cha siasa anatakiwa kutoa taarifa kwa Msajili ndani ya siku 30. Taarifa hiyo ni lazima ielezee malengo na aina ya mafunzo, program ya mafunzo hayo, watu watakaohusika, vifaa vya ufundishaji na matokeo tarajiwa ya mafunzo hayo. Msajili baada ya kupokea taarifa hiyo anaweza kukubali au kukataa uendeshaji wa mafunzo hayo.

Sheria imeanisha kuwa mtu yeyote atakayetoa mafunzo bila kibali cha Msajili atakuwa ametenda kosa na akikutwa na ***hatia atawajibika kulipa faini ya kiasi cha fedha kisichopungua shillingi 500,000/= na kisichozidi shillingi 5,000,000/= au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kwa pamoja.***
***Endapo kosa hilo litakuwa limetendwa na taasisi, adhabu yake itakuwa ni faini isiyopungua kiasi cha shillingi 5,000,000/= na kisichozidi shillingi 30,000,000/=. Pamoja na adhabu hizo mhusika atatakiwa kuwasilisha taarifa zote kuhusu mafunzo hayo kwa Msajili ndani ya muda utakao amuriwa na Msajili.***

#### • Mamlaka ya Msajili kuomba Taarifa

Katika kutekeleza majukumu yake Msajili ameruhusiwa na Sheria kuomba taarifa yoyote ya chama cha siasa au kiongozi itakayotakiwa katika kutekeleza masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Chama cha siasa au kiongozi wa chama cha siasa atakayekaidi maombi hayo atakuwa ametenda kosa na adhabu ya kosa hilo ni ***faini isiyopungua kiasi cha shillingi 1,000,000/= na kisichozidi shillingi 10,000,000/=***. Pamoja na faini hiyo Sheria inamtaka kiongozi au chama cha siasa kutoa taarifa zilizoombwa na Msajili.

### 3.0 Uundaji wa Chama cha Siasa

Chama cha siasa kinatakiwa kufuata misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar, Katiba ya chama husika, misingi ya demokrasia na utawala bora na kisiwe chama cha kibaguzi.
Sheria ya Vyama vya Siasa inavitaka vyama vya siasa pale vinapoanzishwa, vinapotekeleza sera zake, vinapoteua wagombea wa chaguzi na vinapochagua viongozi wake kuhakikisha vinakuza ;-

- Muungano,
- Mapinduzi ya Zanzibar,
- Demokrasia,
- Upingaji rushwa,
- Umoja wa kitaifa,
- Uzalendo,
- Mwenge wa uhuru,
- Amani na utulivu wa nchi.

### 4.0 Sifa za Kuomba Usajili wa Vyama

Sheria imeanisha sifa za mtu ambaye anaweza kuomba usajili wa chama cha siasa kama zifuatazo ;-

i. Awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzaliwa na wazazi wake wote ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
ii. Mtu mwenye akili timamu;mtu ambaye hajatangazwa na mahakama kuwa amefilisika;
iii. Ana umri wa miaka 18 au zaidi;
iv. Anaweza kusoma Kiswahili au Kiingereza na
v. Mtu ambaye ndani ya miaka mitano kabla ya kuwasilisha maombi ya usajili hajakutwa na hatia au kuhukumiwa kwa kosa la kukosa uadilifu, kosa la uhujumu uchumi, rushwa, kukwepa kodi au kosa linalohusiana na unyanyasaji wa kijinsia.

### 5.0 Sifa za Mwanachama

Sheria ainisha sifa za mwanachama wa chama cha siasa. Sifa hizo ni ;-

i. Raia wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania; na
ii. Amefikisha umri wa miaka 18.

Hata hivyo Sheria hii imekataza mtu kuwa mwanachama zaidi ya chama kimoja cha siasa. Mtu yeyote atakayemiliki zaidi ya kadi ya chama kimoja itachukuliwa kuwa ameacha uanachama wa chama cha awali. Sheria pia imekataza mtu ambaye si raia wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa maamuzi ya chama cha siasa kwa nia ya kukuza chama hicho na akifanya hivyo atakuwa ametenda kosa na adhabu yake ni ***faini isiyopungua kiasi cha shillingi 20,000,000/= na kisichozidi shillingi 200,000,000/= au kusimamishwa au kufutiwa usajili wa chama hicho cha siasa.***

Mwanachama wa chama cha siasa hataweza kufukuzwa uanachama wa chama cha siasa bila ya kufutwa kwa utaratibu uliyowekwa katika Katiba ya chama hicho.

### 6.0 Usajili wa Vyama vya Siasa

Sheria imempa mamlaka Msajili wa Vyama vya Siasa ya kukataa usajili wa chama cha siasa endapo chama cha siasa kilichoomba usajili ni wazi kuwa jina lililopendekezwa, kifupisho chake au alama yake ;-

i. Ina maana mbaya;
ii. Linatumiwa na chama kingine cha siasa au
iii. Kilitumiwa na chama kingine cha siasa kilichofutwa.